# UQAB

Jarida la

*Toleo 34 - Rabi-ul-Awal 1441 H / Novemba 2019 Miladi*





**Uingereza – Jamhuri Mpya ya Fujo**

**Uache Ubaguzi**

**Turegeshe Ngao Yetu**

**Kufufua Muundo wa Utawala!**

**Ndoa Za Mapema**

**SWALI/JAWABU Mzozo wa Amerika na Ulaya ndani ya Sudan**




## Zawadi ya Kikoloni kwa Kufaulu Kutekeleza Ajenda za Kikoloni!

# Zawadi ya Kikoloni kwa Kufaulu Kutekeleza Ajenda za Kikoloni!

Siku ya Ijumaa, 11 Oktoba 2019, kamati ya Nobel ilimzawadi Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed Ali kama mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel ya mwaka 2019. Alizawadiwa kwa juhudi zake za kupatikana kwa amani na ushirikiano wa kimataifa na hususan kwa uamuzi wa mpango wake wa kutatua mzozo wa mipaka na nchi jirani ya Eritrea. Zaidi ya hayo, Waziri Mkuu alisifiwa kwa kuzindua mabadiliko muhimu yanayolenga kuboresha demokrasia ndani ya Ethiopia.

Abiy Ahmed Ali, mwanachama wa kabila kubwa la Waislamu la waasi wa Oromo ambaye mamake ni Mkristo Muamharic na mkewe ni vivyo hivyo. Abiy alipewa uongozi na bwanake mkoloni Muamerika ili kunusuru maslahi yake wakati wa vurugu baada ya kuhisi kibaraka wao wa zamani Waziri Mkuu Hailemariam Desalegn ushawishi wake umeshuka na kumtaka kujiuzulu. Hii ni kutokana na kutoweza kusitisha mzozo wa kisiasa ulioshuhudiwa nchini humo uliosababishwa na mpango wa serikali kutaka kupanua mji mkuu wa Addis Ababa na kuchukua ardhi za ukulima zilizokuwa pembezoni mwake.

Ndani ya muda mfupi wa mwaka mmoja na nusu (Aprili 2018 – Oktoba 2019) tangu Waziri Mkuu Abiy Ahmed alipoingia afisini ametekeleza mengi kwa mujibu wa maamrisho ya bwanake Muamerika. Kama inavyofichuliwa na ziara yake ya kwanza kwani alikwenda Saudi Arabia 17/5/2018 kwa mualiko rasmi kutoka kwa Mfalme Salman Bin Abdul Aziz ambaye ni kibaraka mtiifu wa Amerika! Kwa kuongezea mtu wa kwanza kumzuru alikuwa ni Mwana wa Mfalme wa Saudi Arabia, Mohammad bin Salman mnamo 7/6/2018. Baadhi ya mambo makubwa aliyoyatimiza yanajumuisha yafuatayo:

**Kwanza,** kuchangamkia Makubaliano ya Kusitisha Vita yaliyopitishiwa na Amerika na kutiwa saini mnamo 18/6/2000 huko Algiers, Algeria baina ya watawala wake vibaraka ndani ya Ethiopia na Eritrea. Ilikuwa ni muhimu kuchangamkia makubaliano hayo ya miaka 18 kwasababu maslahi ya Amerika ndani ya Ethiopia na Pembe ya Afrika kwa ujumla yalikuwa yanakabiliwa na tishio hatari kutokana na kukosekana utulivu mara kwa mara na hili kimaumbile lilikuwa linaidhoofisha serikali na kuiweka wazi kwa upenyezaji wa kutoka nje kutoka kwa dola za kikoloni kama Uingereza kupata ushawishi wa kisiasa na Uchina kupata ushawishi wa kiuchumi. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kupatikane Makubaliano ya Asmara yaliyotiwa saini mnamo 09/07/2018. Baada ya miezi miwili chini ya udhamini wa Mfalme Salman, Rais wa Eritrea Isaias Afwerki na Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed Ali walitia saini Makubaliano ya Amani ya Jeddah mnamo 16/9/2018. Utiaji saini ulifanyika mbele ya Mwana wa Mfalme wa Saudi Arabia. Hili linathibitisha kwamba yalikuwa ni makubaliano ya kimakusudi yaliyoidhinishwa na Amerika ili kupunguza uzito kwa kibaraka wake wa Ethiopia na kumpa umaarufu kindani na eneo jumla!

**Pili,** kuwasilisha sera ya kiuchumi ya kirongo kwa msingi wa kuwadanganya watu na kuwapa matumaini machache kwa kuzingatia kuwa Ethiopia hivi sasa inataabika katika umasikini licha ya kwamba imo miongoni mwa mataifa yaliyo na uchumi unaokuwa kwa kasi ndani ya Afrika. Hivyo basi Makubaliano ya Asmara yalikuwa ni kuweza kupiga jeki uchumi wa Ethiopia ili kuimakinisha na kupunguza kasi ya maandamano ambayo aghalabu huusisha vijana ambao ni asilimia 50 ya idadi ya Waethiopia waliochini ya miaka 18 ambao kidogo tu wausambaratishe utawala wa Waziri Mkuu wa zamani. Ethiopia ni nchi isiyokuwa na bandari ambayo uchumi wake unategema kwa kiasi kikubwa usafirishaji wa ukulima kwa hiyo ilihatajia kwa dharura makubaliano na Eritrea ili kuweza kupata nafasi kuutumia mwambao wa pwani ya Bahari Nyekundu kama mlango wa kuelekea kwa washirika wa kibiashara wa Dunia na hususan makampuni ya Marekani. Kwa upande mwingine, makampuni ya Kiamerika yamepatiliza nafasi ya kupora rasilimali za Ethiopia kwani imeripotiwa kwamba Ethiopia inayohifadhi kubwa ya mafuta katika maeneo mengi na kazi tayari imeshaanza ya kuchimbua mafuta katika maeneo mengi (Ethiopiana.net 1/4/2013)... "Uzalishaji wa visima vya mafuta ndani ya eneo vinatarajiwa kufikia gallon bilioni 40 za mafuta na kuwasili sokoni mnamo 2018 (Mogadishu Center 25/12/2016). Wakati huo huo, Amerika inajaribu kuipiku Uchina katika ushawishi wa kiuchumi duniani na Afrika, hususan ndani ya Ethiopia ambapo inazingatiwa kuwa ni eneo la viwanda la Uchina ndani ya Afrika!

**Tatu,** kwa kutekeleza sera za Amerika kuhusiana na mipango ya kupambana na ugaidi ndani ya eneo tukizingatia kuwa Ethiopia inalo jeshi kubwa na lenye uwezo ambalo chini ya Meles Zenawi mnamo 2006 liliidhinishwa na Amerika kupigana na harakati za Kiislamu na kupindua utawala wa mahakama za Kiislamu ndani ya Somalia. Jeshi la Ethiopia limebakia ndani ya Somalia mpaka wa leo ili kuhifadhi ushawishi wa Amerika kisiasa na kiuchumi. Makubaliano na Eritrea yanatarajiwa kutia

**Endelea...UK 3**

pondo uboreshaji wa mipango na kupangilia vyema majukumu maalum ya wanachama wa eneo; ya-kijumuisha Djibouti ambayo ni mwenyeji wa kambi ya kijeshi kubwa ya Amerika ndani ya Afrika na ambayo ni muhimu katika kampeni ya Yemen am-bayo Marekani inashirikiana na Saudi Arabia katika kupigana na washirika wa Uingereza ili wasichukua uongozi wa Yemen!

**Nne,** kwa kuleta mabadiliko maovu ya kisanii chini ya pazia ya kuboresha demokrasia kwa jina la kupi-gia debe ukombozi wa wanawake ambapo mnamo Jumanne, 16 Oktoba 2018 Waziri Mkuu Abiy Ahmed alitaja baraza lake la wanachama 20 na huku wanawake wakichukua vyeo hivyo sawa na wen-zao wanaume. Zaidi ya hayo alisema "Wanawake wetu mawaziri watatoa changamoto kwa msemo wa zamani kuwa wanawake hawawezi kuongo-za. Maamuzi haya ni ya kwanza katika historia ya Ethiopia na labda Afrika." Kisha mnamo Alhamisi, 1 Novemba 2018 Waziri Mkuu Abiy Ahmed alimteuwa Meaza Ashenafi , wakili wa haki za binadamu na mwaharakati wa haki za wanawake ili kuwa mwa-namke wa kwanza kusimamia Mahakama Kuu ya Ethiopia.

**Tano,** kwa kutia juhudi za kupatikana kwa maazimio ya amani katika mzozo wa Sudan Kusini kwa man-ufaa ya bwanake Muamerika ambaye ndiye sababu ya kugawanywa kwa Sudan chini ya uongozi wa Omar al-Bashir kabla umuhimu wake kuisha na kupinduliwa! Wakati huo huo akitoa mkono muovu wa upatanishaji baina ya Somalia (kibaraka wa Muamerika) na Kenya (kibaraka wa Muingereza) katika mzozo wa mpaka wa bahari unaoendelea kutokota!

Hizo ni baadhi ya amali zake zilizojaa hila ambazo amezitekeleza tangu kuingia madarakani mnamo 2 Aprili 2018 na anaendelea kumuhudumikia bwa-nake mkoloni Muamerika mpaka hivi leo. Sijambo la kushangaza kwa yeye kupata zawadi hiyo ndani ya muda mfupi tangu kuingia uongozini! Kwa kuwa zawadi haizingatii sifa yoyote kubwa bali inaza-wadiwa kwa wale ambao wanatekeleza kwa ubora mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake za kutamausha na kwa upande mwingine ubora na utiifu katika kuwatumikia mabwana zao wakoloni! Kwa mfano chini ya miezi minane tangu kuingia mamlakani kama rais wa Amerika Barack Obama al-izawadiwa Tuzo ya Amani ya Nobel ya mwaka 2009 kwa 'kuwa rais mweusi kuingia White House!' am-bayo ilikuwa ni njama ya kuweza kuwahadaa watu duniani na kuficha mikono iliyojaa damu ya utawala wa Amerika ambao ulikuwa unaharibu na kupo-ra mataifa mengine na kuua watu wao kama vile vita vya kirongo vya Iraq na Afghanistan ambavyo Barack Obama alivirithi na kuviendeleza mpaka kwa utawala uliopo sasa!

Ni muhimu kufahamu kuwa zawadi kama hizi ni za uhadaifu na zinalenga kuweka msingi ili kuhalalisha upitishaji wa sera na sheria zinazolenga kulinda maslahi ya dola za Kimagharibi za kikoloni zin-azoongozwa na Amerika na washirika wake duniani kote. Zikifanyika kwa kisingizio cha mabalozi wa amani ambao kiuhalisia sio chochote bali ni wam-wagaji damu na hususan damu za Waislamu na kunajisi matukufu yao kama yale yanayoendelea Al-Quds, Kashmir na maeneo mengine!

Kwa kutamatisha ni lazima tuzikatae zawadi kama hizo ambazo malengo yake ni kuwazawadi watawa-la vibaraka masekula ili kununua unyamavu na utiifu wao kwa mabwana zao Wamagharibi wakoloni. Kukataa huko kufuatiwe na kujiunga na kufanyakazi ya ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Ni Khilafah ndio itakayouondosha ukoloni Afrika na duniani kwa ujumla kwa kuondosha minyororo yake katika kila nyanja ya maisha kwa kutekeleza kwa ukamilifu Shari'ah (Qur'an na Sunnah).

**Ali Nassoro Ali**

# Uingereza – Jamhuri Mpya ya Fujo

Uingereza kwa muda mrefu imekuwa katika kilele cha kutawala kiasi kwamba jua halikuchwa na kileleni mwake taifa hili la kisiwa lilitawala zaidi ya asilimia 25 ya watu duniani. Lakini hilo lilikuwa zamani sana na hivi leo Uingereza imeshindwa na mataifa kama Pakistan, Bangladesh na Zimbabwe katika kuonekana kuwa ni mazuri. Kwa kuzingatia kuwa mnamo 2019, India itakuwa na Mapato ya Taifa (GDP) makubwa kuliko UK. India ambayo mpaka hivi majuzi ilikuwa ni taifa la ulimwengu wa tatu, taifa ambalo lilikoloniwa na UK litakuwa na uchumi mkubwa kuliko UK. India inayo kila haki kuiondosha UK ndani ya Umoja wa Mataifa (UN) na katika mazungumzo ya kibiashara. India iliyokuwa imevamiwa na UK itakuwa na umuhimu mkubwa katika uchumi wa dunia kuliko taifa ililolikoloni.  Dunia inabadilika na ndani ya UK kigezo hicho kimeipelekea kutathmini nafasi yake ndani ya Umoja wa Ulaya (EU) na nafasi yake duniani.

Kikundi cha wanasiasa ndani ya Uingereza wamekuwa katika msuguano kuhusu uanachama wake ndani ya EU na kwa namna gani unaisaidia UK. Mgawanyiko huu umesababisha mzozo mkali wa kindani ambao umekuwepo kwa miaka arubaini. Kura ya maoni ilipelekea kushinda kwa wanaotaka kujiondoa lakini kwa miaka mitatu mtawalia wanasiasa wamefanya kila wawezalo ili wasitekeleze maamuzi ya uchaguzi wamechelewesha kuondoka katika EU na wameweka masharti juu ya masharti katika mazungumzo yao na EU na kilichowazi hivi sasa kwa umma ni kwamba kura yao haikuzingatiwa na wanasiasa hawajali matakwa ya watu.

Nafasi ya Uingereza inaonekana lau kama ambaye Uingereza itabakia basi ipate mgao ambao utakaoiwezesha kupata manufaa ya EU, muungano wa forodha na soko moja lakini iweke vikwazo kwa uhamiaji na kujiweka mbali na michakato yoyote ya EU ambayo itakuwa haiwafai. Ikiwa mgao hautopatikana basi Uingereza ni bora iwe nje ya EU. Mazungumzo na EU kuhusiana na hilo yanaelekea kufeli kwani Uingereza inataka mgao maalum ambao hakuna mwanachama aliyenao ndani ya EU.

Tatizo kwa Uingereza ni kwamba hakuna sababu ya EU kujifunga na masharti hayo. Ni kwa maslahi ya EU kuhifadhi EU na kuibakisha Uingereza ndani ya EU kwa kuwa hakuna taifa lililowahi kutoka EU. Ugiriki licha ya kuwa ndani ya kina cha janga la kiuchumi wakati ambapo Ujerumani ilikuwa inaweka masharti makali rai ya umma ilibakia juu kwa Ugiriki kubakia ndani ya EU. Lakini kwa kuwa mazungumzo yamechukua muda wa miaka mitatu wengi ndani ya EU wanaitizama Uingereza kama mtoto mkorofi asiyestahiki kupewa manufaa ya EU.

EU iliipa mgao UK pale ambapo itahitajika kukubali haki ya Wauropa kusafiri kwenda UK nao wairuhusu kuingia katika soko moja na muungano wa forodha. Lakini bunge la Uingereza lilikataa kukubali mgao huo kwa kuzingatia kuwa uhamiaji ulikuwa suala muhimu kwa waliopiga kura ya kujiondoa katika EU. Theresa May aliwasilisha mgao huo mara tatu bungeni kwa matumaini kwamba ungepita lakini alifedheheshwa na kulazimishwa kuondoka afisini.

Boris Johnson aliingia afisini akiwa na mkono dhaifu, EU ilikuwa imeweka wazi kwamba haitokubali kuzungumza tena mgao wowote na kwamba ule aliopewa Theresa May ndio wa mwisho. Johnson aliingia afisini nyuma huku akizingatia kuwa amejiandaa kuitoa UK pasina mgao wowote. Amejaribu kuulazimisha mkono wa EU. Viongozi wa Ulaya kwa muda mrefu wamemtazama Boris Johnson kama ni mjinga asiyemuanifu anayeongozwa na matamanio ya kibinafsi. Serikali zote za May na Johnson zimejaribu kwa muendelezo kutolijumuisha bunge katika kuwa na dori ndani ya mazungumzo ya kujiondoa, huku jaribio la Boris la hivi majuzi ni kuhairisha bunge.

Kujionda katika EU kumefichua uhalisia wa demokrasia, nidhamu ya utawala wa wachache kwa wachache kwa ajili ya wachache. Boris Johnson kiuhalisia anajiandaa kuweka maandalizi ya uchaguzi mkuu usioepukika. Kilicholengwa kuwa ni talaka ya kimya kutoka EU imegeuka na kuwa ni maonyesho ya kila siku katika TV yaliyokuwa na visa vipya ambavyo hakuna anayeweza kuvihimili.

Iwe itakavyokuwa ni wazi kwamba Uingereza ima itabakia ndani au nje ya EU inadondoka katika kikundi cha mataifa makuu, wakati ambapo India hivi karibuni itaitizama Uingereza ikiwa nyuma. Ahadi ambazo kikundi cha wanasiasa ilizotoa kwa raia wake zilikuwa ni porojo tu za kuficha nia zao za kweli.

**Adnan Khan**

# Habari & Maoni
# Uache Ubaguzi wa Rangi kwani Unachukiza



**Habari:**

Mtoto wa miaka 9 wa Syria kwa jina Wael al-Saud, aliyekuwa anaishi katika wilayah ya Kocaeli's Kartepe, alijitoa uhai kwa kujinyonga katika mlango wa makaburi. Imeripotiwa kwamba mtoto huyo mdogo alikuwa amelikejeliwa na mwalimu siku hiyo na kuzomewa kwa ujumla na wanafunzi wengi kwa kuwa alikuwa ni Msyria. (http://www.haber7.com)

**Maoni:**

Moja katika desturi za ujahiliya ambazo zilikuwa zimetawala maisha ya watu wakati wa utawala wa Rasulullah (saw) alipokuwa ametumilizwa kama nabii, ilikuwa ni ubaguzi wa rangi na utaifa. Uislamu ukaondosha chuki hizo wakati wa ujahiliya ambazo zilijitokeza kutokana na tofauti za makabila, "kwa kuwafanya Waislamu ni ndugu" na kuharamisha kudai ubora kwa misingi ya ukabila na kuufunga tu kwa Uchajimungu pekee.

Uislamu ukayeyusha tofauti za ukabila na kuwa umoja mmoja katika chungu cha "Aqeedah ya Kiislamu" na kufundisha udugu. Mwamko wa udugu chini ya Khilafah ukapelekea Waislamu kufaulu kwa miaka. Na makafiri walipogundua kwamba hawawezi kuwashinda Waislamu katika vita wakabuni mipango yao miovu na wakakatikiwa kuwa njia pekee ya kuwashinda Waislamu ni kuivunja Dola ya Kiislamu ya Khilafah ambayo ilikuwa ni kiunganishi cha Waislamu, kwa kupanda mbegu za mizozo na kupenyeza sumu za utaifa na hivyo wakafaulu. Lakusikitisha walifaulu katika mipango yao michafu. Natija yake ilikuwa ni kuvunjika kwa umoja wa Ummah kwa kuigawanya dola moja ya Waislamu na kuwa zaidi ya vijidola 50 vilivyokuwa na mipaka ghushi ya Sykes-Picot. Hili likafuatiwa na uvamizi na uporaji wa ardhi zetu kwa kuongezea mauaji kwani ngao ya kuwalinda Waislamu na imani yao ilikuwa imevunjwa.

Kujitoa uhai kwa mtoto wa miaka 9 wa Syria kwa jina Wael al-Saud ni natija ya mchakato wa historia ya uhamiaji ambayo ilianza kwa uhamiaji miaka tisa iliyopita na kuishia kwa kifo. Mapinduzi ya Syria yalianza takribani miaka 9 iliyopita. Wakati wa mapinduzi, ndugu zetu walijipata katika ulengwaji wa risasi na mabomu kwa nyumba zao na unyama mwingi. Familia nyingi zimesambaratishwa kabisa. Idadi ya watoto wasiokuwa na wazazi na wanawake wajane wamezidi.

Matatizo haya yamepelekea uhamiaji wa ndugu zetu ili kutafuta mazingira yenye ustawi zaidi. Hivyo basi milioni kadhaa ya ndugu zetu Wasyria wakapata makaazi ndani ya Uturuki. Ndugu zetu Wasyria wamelazimishwa kuwacha nyuma nyumba zao na miili iliyokufa ya wenzao ambazo ni mali zetu kama zilivyo mali zao kwa kuwa ni za Uislamu ili kupata

**Endelea...UK 6**

hifadhi kutoka kwetu. Lakini kumekuwa na wakati ambapo walichomwa kwani nyumba zao zilipoporwa na wakati mwengine walikuwa waathiriwa wa mauaji. Ukandamizaji walioukimbia ndio unaoendelea kuwakumba ndani ya bandari ya salama waliyokuwa wakiitafuta.

Hivyo basi, nani anaweka msingi huu wa rai amma dhidi ya ndugu zetu Wasyria? Kwa maana nyingine ni nini sababu ya uadui dhidi ya Wasyria? Ni wazi kuwa dola ya Uturuki iliyobeba siasa za utaifa za uhamiaji ndio wanaoulingania.

Ndiyo, yanayojiri kutokana na siasa mbaya za utaifa, hatua ya ukandamizaji kutoka kwa serikali tawala na vyombo vyake vya habari wamejidhihirisha ndani ya mujtama kwa muda mfupi. Ujenzi wa rai amma dhidi ya Wasyria imeandaa mazingira ya ufurushaji wa ndugu zetu wahamiaji Wasyria. Hisia za chuki dhidi ya Wasyria miongoni mwa umma, mtazamo wa kejeli unaoashiria "nenda zako!" na kufanyiwa maudhi kumezidi. Vitendo vya kinyama vimechipuza ambavyo vimewalenga wanawake na watoto, Wasyria wanalaumiwa pasina shutuma zilizo na msingi wakifuatiwa na kuvamiwa kupitia kuporwa na kuchomewa nyumba zao Wasyria.

Kujitoa uhai kwa mtoto wa miaka 9 wa Syria kwa jina Wael al-Saud ni mfano wa hivi karibuni. Kwani ripoti zinasema kwamba Wael al-Saud alifanyiwa kejeli na wanafunzi wenziwe na mwalimu siku hiyo ya kujiua. Lau hilo ni kweli, basi kujiua kwa mtoto huyu sio tu tukio la kujiua bali ninapendekeza lizingatiwe kuwa mauaji na watekelezaji wake wanajulikana. Watekelezaji hawa waliompelekea mtoto wa miaka 9 kujiua ndio walinganizi wa utaifa wabaguzi wa rangi ambao wanachukia uwepo wa Muislamu wa rangi nyingine na wanasiasa walinganizi wa utaifa ambao kila mara wanachochea uadui na chuki kwa matamshi yao dhidi ya Wasyria na uhamiaji na baadhi ya mashirika ya habari ambayo hayajui mipaka wakati wa kushambulia Uislamu.

Haya ni madhambi na ni madhambi ya wale wanaochochea ubaguzi wa rangi. Ni madhambi ya wale wanaopanda hisia za uadui badala ya kuwa Ansar. Ni madhambi ya wale wanaotaka kuendeleza dhati ya Sykes-Picot badala ya dhati ya Ummah. Kwa ufupi haya ni madhambi ya wale ambao nafsi zinawataka Wasyria kuondoka.

Sasa ndio wakati wa kuwa Ansar wa karne hii kwa ajili ya Waislamu Wasyria ambao wametafuta hifadhi kwetu – ndugu zao – ili kukimbia maangamivu na ukandamizaji walimokuwa wakiishi. Leo ndio siku ya kuwa Ansar ambao walimkubali Rasulullah (saw) wakati wake wa shida na kumnusuru yeye (saw) na Dini yake kwa kumpa nguvu na utukufu.

Katika hadith ndani ya Al-Bukhari, Rasulullah (saw) asema:

«الْمُسْلِمُ أَخُو الْمُسْلِمِ لَا يَظْلِمُهُ وَلَا يُسْلِمُهُ وَمَنْ كَانَ فِي حَاجَةِ أَخِيهِ كَانَ اللَّهُ فِي حَاجَتِهِ»

"Muislamu ni ndugu ya Muislamu mwengine, kwa hiyo hatakiwi kumkandamiza, wala hatakiwi kumsalimisha kwa mkandamizaji. Yeyote atakayekidhi haja za nduguye, Mwenyezi Mungu atamkidhia haja zake."

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Abdullah İmamoğlu**

# Wilayah Pakistan: Turegeshe Ngao Yetu!

Turegeshe Ngao Yetu, Khilafah ili Majeshi Yetu Hatimaye Yaweze Kupaza Sauti za Takbeeraat za Ushindi ndani ya Srinagar na Al-Aqsa

Utawala wa Bajwa-Imran unamaanisha hatua ya kuchukuliwa ni ile ya hotuba tu, ilhali hitajio la wakati ni moto, damu na chuma.

Kando na kutambua kwamba Kashmir ni mshipa wa shingo zetu, utawala wa Bajwa-Imran umezuia vikosi vyetu vyenye uwezo ili visivuke Mstari wa Udhibiti ili hatimaye kwa nguvu kuyafurusha majeshi ya India ya uvamizi yaliyokata tamaa na yanayo dorora.

Licha ya kutambua ujasiri wa Waislamu watukufu wa Kashmir, utawala wa Bajwa-Imran umefanya kuwa mwito kwa Jeshi la Pakistan kuwakomboa kuwa ndio kauli mbiu ya “ugaidi,” kwa mujibu wa nakala ya FIR iliyotolewa dhidi ya Hizb ut Tahrir mnamo 1 Oktoba 2019 ikiwa na nambari ya utambuzi RWP-WAK-002476.

Enyi Waislamu wa Pakistan na hususan Wanajeshi!

Tusiwe na shaka kwamba ni mpaka tutakaporegesha Khilafah yetu kwani watawala Waislamu waovu wataendelea kupoteza muda huku maadui zetu vitani wanatuvamia ima ni katika msalaba, India au umbile la Kiyahudi.

Kwa hiyo wafungueni simba wetu wanajeshi wa Pakistan kutoa Nussrah (msaada wa nguvu) ili kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume, ili waweze kuongozwa kama wanavyostahili kutafuta ushindi au shahada…

**Jumatatu, 08 Safar 1441 H - 07 Oktoba 2019 M**



# Enyi Waislamu, Ngao ya Frati, Tawi la Mzeituni na Chemchem ya Amani Zote ni Hatua katika Msururu wa Kufufua Muundo wa Utawala!

Aliyoyafanya na anayoyafanya Erdogan ni kutekeleza yale ambayo Amerika inayataka; kuimarisha utawala wa kidhalimu ndani ya Syria kwa kutumia mikono miovu ya kimataifa, kimaeneo na mashinani. Hii ni baada ya kelele za watu na uasi wao uliposhtua utawala na Amerika nyuma yake na washirika wake kutoka Urusi, Iran na Erdogan wa Uturuki na makundi yake na kupanga njama ili kutekeleza mipango ya Amerika ili kuimarisha nidhamu iliyokita ya Kisekula ndani ya mji wa Ash-Sham! Tayari tulitoa Jibu la Swali mnamo 7/12/2016 kuhusu njia za udanganyifu za Erdogan katika Ngao ya Frati na Tawi la Mzeituni ambalo lilifichua uhalisia wa wale waliodanganywa na kuvutiwa na matamshi ya Erdogan wakifikira kuwa anawaunga mkono dhidi ya dhalimu wa Syria, lilisema: (Kuongezea hili ni muendelezo wa kampeni ya Erdogan ya Oparesheni ya Ngao ya Frati na jaribio lake la kuvutia makundi mengi ya kijeshi upande wa Uturuki katika vita vya Al-Bab baada ya Jarablos yote haya ni kwa ajili ya kudhoofisha safu za kweli za Aleppo ambayo yalitegemewa ili kuiondosha na kuiokomboa kutoka katika kizuizi cha kuzungukwa). Na hivyo basi Aleppo ikapotezwa! Makundi hayo yalitakiwa yawe yamejifunza lakini kwa mara nyingine yameumwa tena katika tundu linalomilikiwa na Erdogan! Waliungana naye kwa mara nyingine katika Tawi la Mzeituni na tukatowa Jibu la Swali wakati huo mnamo 24/1/2018, ambalo lilisema: (Hivyo basi Erdogan anarudia hali ya Ngao ya Frati ili kuuwezesha utawala kuingia Idlib. Oparesheni ya Tawi la Mzeituni ikapangwa ili kuuwezesha utawala kuingia Idlib).

Jibu la Swali jengine lilitolewa mnamo 29/07/2018 lilisema: (Ngome ya pili: iliongozwa na Uturuki katika vita vya Ngao ya Frati kaskazini mwa Aleppo mnamo 24/08/2016 na kisha Tawi la Mzeituni mnamo 20/01/2018 ikaifanya kuwa ni rahisi kwa utawala kuingia Aleppo na kusini mwa Idlib. Ni kwa sababu makundi haya yaliamrishwa na Uturuki na kuondoka vitani dhidi ya utawala na kwenda kupigana katika kampeni ya ngao na tawi, Aleppo na Idlib kusini zikapotezwa au zikakaribia kupotezwa!) Hivi sasa makundi yamefanywa wajinga kwa mara ya tatu kwa Oparesheni ya Chemchem ya Amani! Kampeni hii imeufufua utawala na kuuzidishia kufaulu kwake kwa agizo la Trump na uungaji mkono: [(Muandishi na mchanganuzi wa kisiasa wa Uturuki, Javad Gok, alisema kwamba "pasina na uungwaji mkono na Amerika" Uturuki haiwezi kusonga mbele ndani ya mashariki ya Frati… (tamuz-net 6/10/2019)]. White House ilitangaza kwamba [(Majeshi ya Amerika yatajitoa kutoka Syria kaskazini huku Uturuki ikijiandaa kuzindua oparesheni ya kijeshi huko, hii ni baada ya mazungumzo ya simu baina ya Rais wa Amerika Trump na mwenziwe wa Uturuki Erdogan. (CNN Arabic 7/10/2019)]. Akithibitisha maagizo ya Amerika na kutafuta kuiridhisha: [Msemaji wa White House alitangaza mnamo Jumanne, ziara inayotarajiwa ya Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan kwenda Amerika mnamo 13 Novemba…(Al-Mashhad Al-Araby, 8/10/2019)]

Ama kuhusu kauli ya Trump kuhusu vikwazo na vitisho [Rais wa Amerika Donald Trump aliiwekea Uturuki vikwazo mnamo Jumatatu na kuitaka kwamba isitishe uvamizi wake wa kijeshi ndani ya Syria kaskazini…(Reuters 15/10/2019)], kauli hizi ni za kudanganya tu na kupotosha kwa sababu inawezekana vipi Trump kumuunga mkono Erdogan na aendelee na kampeni yake kisha amtishie kwa vikwazo na kumuagiza kusitisha kampeni yake? Isipokuwa ni maagizo ya Trump kwa Erdogan yanakaribia kuisha na hivyo basi vikwazo ni njia ya kutokea tu! Hivyo basi Erdogan alitekeleza kampeni yake kwa maagizo ya Amerika na atasitisha kwa mujibu wa mipaka aliyowekewa kufika, ima amejipatia kitu au la kwa kuwa lengo ni kutekeleza mipango ya Amerika kwa kuyarudisha maeneo ambayo yalikuwa hayadhibitiwi na utawala kuyarudisha kwa utawala. Na hivyo rasmi kutambuliwa kama umbile kieneo na kimataifa! Kauli za watu zinadhihirisha hilo kwa uwazi: Muungano wa kimataifa ulithibitisha mnamo Jumanne kwa mujibu wa Kanali Myles B. Caggins, msemaji wa Oparesheni Asili ya Kutatua (OIR) katika ya muungano huo katika Twitter…(Arabi21, 15/10/2019)].

Kwa mujibu wa kauli ya Wizara ya Ulinzi ya Urusi kwamba (jeshi la serikali ya Syria linaudhibiti kamili wa mji wa Manbij na viunga vyake…(France 24 / AFP 15/10/2019))…Erdogan alizingatia kuingia kwa jeshi la Syria ndani ya Manbij kuwa ni jambo zuri na sio baya! [(Erdogan alisisitiza kwamba kuingia kwa jeshi la Syria ndani ya mji wa Manbij sio vibaya…...(Al-Arabiya 16/10/2019)]...Makamu wa Rais wa Amerika alisema kwamba: [ataongoza ujumbe kwenda Uturuki hivi karibuni, na kwamba Rais wa Amerika amezungumza na mwenziwe wa Uturuki Erdogan na kumtaka kusitisha mara moja uvamizi wa Uturuki ndani ya Syria…(Al-Ghad Channel 15/10/2019)]...

Gazeti la Uturuki la Jumhuriyat lilisema kwamba Waziri wa Ulinzi wa Uturuki Akar aliripoti [kwamba Ankara inatafuta njia za kuwasiliana na utawala wa Syria…(Arabi21 15/10/2019)]. Moscow ilitangaza

**Endelea...UK 9**

kwamba [serikali za Damascus na Ankara zimo katika mazungumzo kufuatia oparesheni za kijeshi za Uturuki kaskazini mwa Syria…(Petra) Ammon Agency 15/10/2019)]. Hivyo basi kampeni ya Oparesheni ya Chemchem ya Amani inaipatia utawala mafanikio mapya, na kuliimarisha umbile lake na kuweka utangulizi kuhusiana na mazungumzo juu yake ambayo yote hayo yasingelifaulu isipokuwa kupitia kampeni hizi ovu!

Yote hayo yanaonyesha kutolewa muhanga kwa watu wa Syria na damu zilizomwagwa na heshima ilivyokiukwa na wahalifu, wanaowafuata, wanaowaunga mkono na zana zao…hazina uzito wowote wala thamani kwa watu ambao wanakwenda mbio kuiridhisha Amerika na mipango yake! Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali inakuwaje wanahadaika. Wanafikiria kwamba kupitia vitendo hivi watawarudisha tena nyuma watu wa Syria katika mikono ya madhalimu washirika wa makafiri wakoloni…Bali kundi la urongo litavunjwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na watakimbia ilhali hawajafaulu chochote kwa sababu walionyanyuka wanataka kuleta nuru inayolingania: “Ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu…” Watu kama hao hawato shtushwa kwa dhiki bali watapa nguvu juu ya nguvu na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wako katika njia iliyonyooka na hawatojisalimisha katika ukandamizaji na hawatojisalimisha katika fedheha lakini ni wanaume wa wanaume wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao katika hali nzuri na mbaya. Na wanapata motisha kutoka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu (swt) na maisha (Seerah) ya Nabii Wake (saw) kama walivyo Maswahaba katika kuendelea kufanya kazi kuwaondosha madhalimu na kusimamisha Sheria ya Mwenyezi Mungu, Khilafah Rashidah. Kila maisha yanapokuwa magumu kwao, yanafuatiwa na wepesi; kila uzito hufuatiwa na wepesi. Kila Amerika na wanaomuunga mkono wanapofikiria kwamba ushindi upo mikononi mwao, mara wanazinduka na kuona kwamba mambo ni makubwa kuliko walivyofikiria na kwamba vitendo vyao vimechanganyikiwa na kauli zao zinakinzana!

Yeyote anayefuatilia mambo atasoma somo na sio tu somo lolote bali ni kuwa mzozo wa kimataifa ndani ya Syria kama ambaye haupo kamwe na hata kimaeneo na mashinani kwa sababu Amerika imedhibiti yote hayo, ilhali Amerika haijafaulu kuweka utawala ndani ya Syria na kumakinisha athari yake kwa miaka kumi ya kusajili wanajeshi wao na zana zao mpaka sasa! Yeyote anayeweze kufikiria kwa makini kuhusu suala hili anajua kuwa batil lazima ishindwe hata baada ya muda mrefu hata lau madhalimu watafaulu mzunguko huu watafeli mizunguko ijayo na siku za hali tofauti zitabadilika miongoni mwa watu…

Kwa kutamatisha, Hizb ut Tahrir inawalingania kwa mioyo iliyojaa ikhlass na ukweli na roho ambazo zinadhuriwa na yale yanayowadhuru na kufurahishwa na yale yanayowafurahisha na kwa sauti zilizochoka ambazo zimekuwa zikiwapa ushauri na muongozo kuelekea njia ya sawa. Kwa hiyo musiwawache vijana wenu katika makundi na walio nje ya makundi kufanywa wajinga na Erdogan na wengine… Ukweli uko wazi kwa watu wote wauone. Kwa hiyo endeleeni na harakati za mabadiliko ili kuondosha tawala za ukandamizaji kwa kufanya kazi ya ukweli na ikhlass na tuko pamoja nanyi lakini kuziongoza safu zenu na kuweni na yakini kwamba Mwenyezi Mungu atanusuru wanaoabudu wakweli licha ya baada ya:

(إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ)
“اHakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi” [Ghafir: 51]. Ushindi sio tu unapeanwa kwa Mitume, lakini pia (والَّذِينَ آمَنُوا) “na wale walioamini”. Ushindi sio tu kwa Akhera, lakini pia (فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ) “wakati wa maisha ya duniani na Siku ambayo mashahidi watasimama”. (إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً) “Hakika, Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake” [At-Talaq: 3].

**17 Safar Al-Khair 1441 H**
**16/10/2019 M**

# Je ni kweli wanakataa “ndoa za mapema”?!



*“Ndoa ya mapema ni tabia ya aibu.” “Ndoa ya mapema ni msiba kwa mvulana na msichana.” “Ndoa za mapema hupelekea matatizo ya kiakili, kiafya na kifamilia na kupoteza haki za watoto.”* Kauli hizo ndizo zinazojirudia mara kwa mara katika semina na makongamano yanayofanywa na taasisi za wanawake au vituo vya haki za binadamu. Na hata katika mabunge ya nchi nyingi wanapotunga sheria za familia mara nyingi huwa wanaongeza umri wa kuoana au wanapendekeza sheria ya kuzuia ndoa kwa vikundi vya vijana kwa umri maalum.

Mashirika ya wanawake – yanayoshirikian na nidhamu zinazowadhamini za Kimagharibi – hupangilia semina ambazo huwaonya dhidi ya ndoa za mapema, wakilingania wazazi wapigane nazo na hata kutaka sheria zinazozuia ndoa za “wasichana waliovunja ungo.” Hili lilitokea Misri, ambayo iliweka umri wa ndoa ni kutimu kwa miaka 18 kama ilivyo katika tovuti ya bunge la Misri mnamo 9/9/2017 ambayo inasubiri kujadili sheria itakayowasilishwa Bungeni ili kuzidisha umri wa ndoa kuwa miaka 21. Hili pia limefanyika ndani ya Morocco ambayo iliweka umri kuwa miaka 16 kwa wasichana na miaka 18 kwa wavulana. Kwa hiyo umri wa kisheria imekuwa ni moja ya masharti ya ndoa ambapo ndoa haiwezi kukamilika ikiwa hautimu. Hii ni kwa mujibu wa makubaliano ya Kimagharibi yanayokwenda sambamba na haya kama makubaliano ya CEDAW ambayo yamejifunga juu ya kanuni na sheria zinazohusiana na kanuni za mahusiano ya wanawake na wanaume. Pia yanatakiwa kutekelezwa na dola zilizotia saini na ziweke sheria zinazokwenda sambamba ndani ya nchi hizo. Lakini swali ni: kwani haya makubaliano ya kimataifa yanalenga kuzuia ndoa za mapema na kuzitizama kama uhalifu dhidi ya watoto na ukiukaji wa haki zao ambazo hutekelezwa kiasili?

Kwa mujibu wa Gazeti la “Al-Sharq Al-Awsat” mnamo 18/5/2010 kwa kichwa: Idadi hii kubwa ya watoto wenye mimba” ilitaja “Idadi ya kina mama wenye mimba ambao hawajaolewa ni zaidi ya asilimia 70 kuliko ile ya kina mama walioolewa, Asilimia 55 ya watoto wanawake 1,000 wana mimba. Asilimia 68 ya watoto waliozaliwa UK ni kutoka kwa wazazi ambao hawakuoana. Chaneli ya MBC iliripoti mnamo 23/1/2012 kuhusu ripoti ya mabarobaro wenye mimba kwa kichwa “Kiwango kikubwa duniani na umri wao ni baina ya miaka 15 na 19: Mabarobaro

**Endelea...UK 11**

Waamerika wanazaa watoto elfu 400 kwa mwaka nje ya ndoa," ikisema kwamba Amerika ndiyo iliyo na idadi kubwa ya wanaozaa miongoni mwa mabarobaro wasichana ndani ya ulimwengu ulioendelea." MWISHO.

Takwimu zinazofichua idadi ya watoto ambao wanahangaishwa, wanabakwa, mahusiano ya watoto shuleni ndani ya Amerika na wasichana walio na mimba ndani ya shule za Kimagharibi ni kubwa mno na hakuna hakuhitajii kuelezea kwa mapana.

Hivyo basi, makubaliano yote ya kimataifa ambayo yanatekelezwa kwa msaada wa serikali za vibaraka ndani ya ardhi za Waislamu na tukizingatia kuwa ni sheria kamilifu za kupangilia mahusiano ya familia na mahusiano ya Waislamu wanaume na wanawake sio sahihi kwa wale waliotuwekea na sio jambo la kushangaza kwa sababu yule ambaye hana kitu hawezi kuwapa wengine kitu. Inawezekanaje kuchelewesha umri wa ndoa katika nchi zetu ilhali wao wanasambaza tembe za kudhibiti mimba kwa wanafunzi shuleni mwao ili kupunguza viwango vya watoto wanaozaliwa kwa uzinifu?? Au midomo yao inaficha yale ambayo mioyo yao inaficha?

Na wafikishia kauli inayohusiana na mada hii, nikifupisha shambulizi juu ya ndoa za mapema licha ya kuwepo kwa sheria za uhuru wa kibinafsi zilizowekwa na makubaliano hayo hayo yanayofanya ndoa za mapema ni uhalifu. "Sio jambo la mzaha na kuhuzunisha kwa wakati mmoja kuzindua neno "ndoa za watoto" kwa ndoa za wasichana wa umri wa miaka 17 na hata kuzingatia kuwa ndoa hii ni janga kwa msichana na wakati huo huo mwili wa msichana ukazingatiwa kuwa ni wake pekee na kwamba ana uhuru wa kuutumia kivyovyote anavyotaka na kwamba hakuna mtu ana haki –yeyote atakayekuwa- kumdhibiti yeye msichana na mtizamo wake wa kijinsia hata kama ni babake au mamake lakini anayo haki ya kuwalaumu wazazi wake wanapo muudhi na kuingilia uhuru wake binafsi?"

Vita dhidi ya ndoa za mapema sio natija ya leo, bali ni tukio katika msururu wa masuala yaliyobuniwa ndani ya vita dhidi ya Uislamu na hukmu zake. Lakini, tutazitafsiri vipi ndoa za mapema kuwa ni hatari kwa afya ya mtoto wakati anapokuwa ana mimba ilhali ipo sheria chini ya makubaliano ya CEDAW na mengineyo ambayo yanawataka mabarobaro wenye mimba kuendelea na elimu zao pasina kulaumiwa na kubeba mimba za uzinifu pamoja na kupitisha sheria ili kupambana na mimba za uzinifu na kumpa chaguo msichana ima kuiavya mimba au kuibeba?

Mashtaka na majadiliano ya kirongo yanadhihirisha kuwa si sahihi kiutabibu na kiuhakika na kwamba kilichofanywa kuwa batili kwa ushahidi wa kukata na takwimu za viwango vya kujifungua, vifo na umri wa mama sio chochote bali ni kelele za mzaha zinazolenga sio kuwalinda watoto au kuwakomboa wanawake bali ni kuweza kuwarahisisha wanawake. Kwa uwazi zaidi ni juhudi kubwa za kuupiga Uislamu na hukmu zake zinazohusiana na familia na kuulinda mujtama kutokana na majanga ya ufisadi na uchafu. Na kila mtu anayeunga mkono au kuhalalisha sio chochote bali ni kuudunga moyo wa Ummah. Sijawasaza hapa wale wanaojaribu kuoanisha vipengee vya Uislamu au kuvitafsiri ili viendane na sheria za kimataifa. Ndoa za mapema zinaruhusiwa ndani ya Uislamu; ni hukmu ya Mwenyezi Mungu (swt) na haistahili kwa mtu yeyote kuikejeli au kuipima kiakili kwa kisingizio cha kuilinda Dini ya Mwenyezi Mungu (swt)

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bayan Jamal**

# Jibu la Swali
# Mzozo wa Amerika na Ulaya ndani ya Sudan



**Swali:**

Imebainika kuwa maafisa wa Ulaya wamemiminika ndani ya Sudan na kutangaza kuinusuru serikali ya Hamdouk. Mnamo 16/9/2019, Waziri wa Kigeni wa Ufaransa aliwasili Khartoum na kukutana na Waziri Mkuu wa Sudan, Abdallah Hamdouk na kutangaza msaada wa Uro milioni 60 kwa Sudan na kwamba itafanyakazi kuiondosha Sudan katika orodha ya Ugaidi. Waziri wa Kigeni wa Ujerumani naye akawasili na kutangaza vivyo hivyo kuhusu orodha ya Ugaidi…

Je mawasiliano na misaada hii ni kuuimarisha muungano wa Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko mbele ya jeshi? Au ni kwa malengo mengine? Waziri Mkuu wa Sudan Abdullah Hamdouk alitangaza mnamo 5/9/2019 kuundwa kwa serikali ya kwanza tangu kupinduliwa kwa Bashir mnamo Aprili (serikali itafanyakazi kwa miaka mitatu ya kugawanya madaraka iliyotiwa saini mnamo mwezi uliopita baina ya jeshi na raia… France 24, 5/9/2019) Je makubaliano ya kugawanya madaraka yanatarajiwa kutuliza au vurugu zitarudi tena kwa mara nyingine?

**Jibu:**

Ili kuweka wazi jibu tunatathmini yafuatayo:

1- Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko kwa msaada wa Uingereza, vyombo vyake vya habari na vibaraka wake wa eneo waliweza kuyateka nyara mapinduzi kutoka kwa watu ambao waliasi dhuluma, njaa, kunyimwa na ufisadi na kurudi nyuma na wala ha-

**Endelea...UK 13**

wakuweza kuweka suluhisho msingi kutatua masuala hayo bali ilitoa suluhisho kutoka ndani ya uhalisia uleule ulio na ufisadi. Mazungumzo yalifanyika baina ya baraza la kijeshi lililoegemea mrengo wa Amerika na vibaraka wake na Ulaya ikipigia upatu Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko. Makubaliano sainiwa baina yao juu ya hati ya kikatiba mnamo 17/8/2019... Kwa hivyo waandamanaji walijitoa muhanga pasina mafanikio. Makubaliano hayo yalikuwa ni muendelezo wa uhalisia wa ufisadi kwa misingi ya Umagharibi usekula dhidi ya Uislamu na hukmu zake! Makubaliano baina ya Baraza la Kijeshi na Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko yalijumuisha wanachama 11 Baraza la Ubwana kwa mgao wa 5+5 pamoja na raia huru ambaye atakubaliwa na pande husika wakati wa mpito kwa muda wa miezi 39.

Makubaliano pia yalisema kwamba Baraza la Kijeshi litachukua hatamu ya kwanza kwa muda wa miezi 21 na Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko yatachukua hatamu kwa miezi 18. Muda wa mpito utafuatiwa na uchaguzi mkuu na kubuniwa kwa baraza utungaji sheria. Makubaliano hayo yalisema kwamba uchaguzi wa mawaziri wa ulinzi na usalama wa ndani uwe ni haki ya kitengo cha usalama cha Baraza la Ubwana kwa maana kuwa kitengo hicho kitabakia chini ya jeshi, usalama na ujasusi kando na kusimamiwa na Baraza la Ubwana kwa muhula wa kwanza.

2- Hivyo basi, nguvu za jeshi lililoko uongozini zinajumuisha sehemu asili ya jeshi. Wapo wanachama watano wa jeshi katika baraza na wawili katika baraza la mawaziri (waziri wa ndani na waziri wa ulinzi). Mmoja ni Jenerali Jamal al-Din Omar, Waziri wa Ulinzi wa Serikali ya Mpito, akiwa ni mmoja wa wanajeshi wakongwe wanaotumikia jeshi hivi sasa. Jenerali Jamal al-Din Omar alikuwa ni rafiki wa karibu wa waziri wa ulinzi, Awad bin Auf aliyefanyakazi kwa muda mrefu ndani ya Huduma ya Kijeshi ya Kijasusi na wenziwe katika Chuo cha Kijeshi walikuwa ni Abdel Fattah al-Burhan na Mkurugenzi Mkuu wa Kijasusi, Abu Bakr Dumblab na Omar Zain al-Abideen. Hii inamaanisha kuwa utawala wa mwanzo utawakilishwa kwa nguvu kwa muhula wa mpito na utaweka vikwazo na vizingiti vingi katika kufaulisha malengo ya serikali ya raia ya Ulaya “Uingereza”… Na hivyo basi upande wa Amerika utabakia wenye nguvu…

3- Abdullah Hamdouk, aliye na mastaz na doktoreti katika uchumi kutoka Chuo cha Uingereza cha Manchester na aliteuliwa na Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko kama Waziri Mkuu mnamo 20/8/2019 napia mamlaka kamilifu yakapewa Baraza la Mawaziri. Mnamo 5/9/2019 kukatangazwa uundwaji wa serikali inayotarajiwa kuongoza muhula wa mpito kwa miezi 39. Hivyo basi Waziri Mkuu atakuwa mtiifu kwa Uingereza na Ulaya na atatenda kwa mujibu wa muongozo wa Ulaya kinyume na Mwenyekiti wa Baraza la Ubwana na Kamanda wa Jeshi Abdel Fattah Al-Burhan na naibu kamanda wa Vikosi vya Msaada wa Haraka Mohammed bin Hamdan Daglo pamoja na wanajeshi wanaogemea mrengo wa Amerika ambao watafanyakazi kwa muongozo wa Amerika.

4- Utawala ndani ya Sudan kwa mujibu wa hati ya kikatiba inakaribia kujumuisha timu mbili zilizo na nguvu na utiifu wa kigeni tofauti na hili litajidhihirisha katika utendajikazi wao katika kusuluhisha matatizo ya watu na usalama wa maisha yao. Kila mmoja atakuwa na hamu ya kuhudumikia muongozo anaoufuata na kila mmoja atasubiri kupatikane fursa kumuondosha mwenziwe kwa kutumia njia za kindani na kinje. Kubuniwa kwa mabaraza kama hayo ndani ya Sudan inajulikana kutokana na mahusiano ya mpito na majanga yake…mpaka pale jeshi litakapopangilia mambo ya dola na kuvunja baraza na kumuweka rais wa nchi kutoka katika maafisa wa kijeshi.  Hili liko wazi kutoka kwa Baraza la Ubwana mnamo 26/12/1955 ambalo lilichukuwa madaraka baada ya “uhuru” wa Sudan mnamo 1/1/1956. Uliendelea mpaka 17/11/1958, wakati Luteni Jenerali Ibrahim Aboud alipokwenda kinyume dhidi yake…and kutokea kwa mapinduzi ya Nimeiri mnamo 1969 kisha mapinduzi ya Omar Al-Bashir mnamo 30/6/1989... Kisha kupinduliwa kwa Al-Bashir na kuundwa kwa Baraza la Ubwana… Mabaraza haya daima yamehusishwa na mizunguko ya mizozo baina ya Amerika na Muingereza na kila mmoja akiwa makini kuunda serikali pekee lau itakuwa hawezi basi hujiunga na mwengine mpaka pale atakapopata nafasi ya kumuondosha mwengine kama ilivyokuwa hapo zamani wakati Amerika ilikuwa kimya kuhusu uwaziri mkuu wa mrengo wa Muingereza Sadiq al-Mahdi ili kuweza kuzimeza harakati maarufu wakati huo na ilipofaulu ili waagiza wanaume wake jeshini kisha wakaja kumpindua Al-Bashir mnamo 1989.

Na wakati Al-Bashir aliposhindwa kudhibiti harakati maarufu ikamuondosha kama ilivyofanya waliomtangulia, Nimeiri na Mubarak na wengine pasina kuzingatia huduma walizotoa! Baada ya Al-Bashir Amerika ilikuja na Baraza la Kijeshi… Na sasa mchezo unarudiwa tena katika Baraza la Ubwana, kwa hivyo jeshi la mrengo wa Amerika lazima kukubaliana na vibaraka wa Uingereza wa Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko ili kumeza hasira za watu ambao Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko waliweza kuzidandia wimbi lake. Walikubaliana kuwahusisha Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko katika serikali lakini mara hii sio sawa na hapo awali, jeshi halikukabidhi serikali yote kama ilivyofanya wakati wa Sadiq al-Mahdi bali ilibakia kama kichwa chake kwa jina la Baraza la

**Endelea...UK 14**

Ubwana na kushikilia vyeo na nafasi muhimu serikalini hata kama nguvu nyingine za ushawishi zilipewa serikali. Baraza la Ubwana ambalo laiongoza nchi nusu yake imejumuisha jeshi na inaongozwa na kamanda wa jeshi Al-Burhan kwa miezi 21 na mawaziri wa ulinzi na usalama wa ndani wamechaguliwa kutoka kwa jeshi ili kuhifadhi uongozi wa kijeshi na usalama wake.

5- Lipi linalotarajiwa? Amerika na Uingereza hawatokaa pamoja kwa utulivu. Maslahi yao ni tofauti na zana zao za mashinani zinafuata hivyo, kwa hiyo kila upande utafanyakazi ili kusitisha harakati za mwengine! Kwa kufuatilia matukio ya sasa, kuyasoma masuala yanayohusiana nayo na kutathmini kauli za kinje na kindani hususan maafisa wa Amerika na Uingereza tunaweza kufahamu njia ambazo kila upande utatumia ili kuhangaisha mpinzani wake na kuweza kumuondosha madarakani kama ifuatavyo:

Ama kuhusu timu ya kijeshi kwa makusudi itaihangaisha serikali kwa upande wa kiuchumi; moja katika sababu muhimu za harakati za watu dhidi ya Al-Bashir ilikuwa ni hali mbaya ya kiuchumi. Serikali ya sasa iliwaahidi watu kuboresha hali ya kiuchumi na lau itafeli basi hili litawafanya watu kuamka tena na itakuwa ni nafasi ya jeshi kuyaondosha Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko kwa maana kuondosha dori ya Ulaya ndani ya Sudan na vigezo vya udhibiti wa uchumi viko mikononi mwa Amerika kama ifuatavyo:

a- Hamdouk alisema katika kongamano la wanahabari pamoja na Waziri wa Kigeni wa Ujerumani: ("Tatizo la kiuchumi la Sudan ni tatizo kubwa, suala la mfumko na ubadilishanaji wa sarafu ya kitaifa na kurudisha ujasiri kwa nidhamu ya benki," na kuongeza: "Mpaka kuwepo na makubaliano na Wshington kuhusu kuiondosha Sudan kutoka katika orodha ya Ugaidi, kutakuwepo na uzito," Anadolu, Reuters 3/9/2019, Hamdouk alisema: ("Kurudisha mawasiliano na Washington ni kipaombele chetu baada ya kuondosha vikwazo kwa kuanguka utawala wa zamani" Anadolu, 8/9/2019 na hivyo basi serikali inahitaji Amerika kuiondoshea vikwazo.

b- Amerika ilianza kwa kuitishia kwa kuwa na msimamo mgumu katika kuiondoshea vikwazo. Baada ya kusaini hati ya kikatiba ambayo vibaraka wake walilazimishwa kuisaini ili kutuliza mabarabara, Amerika ikaanza kurudi nyuma katika kuiunga mkono Sudan. Ubalozi wa Amerika ndani ya Khartoum ambao muhula wake uliisha, uliwajulisha watu maarufu wakuu ndani ya Sudan kwamba suala la kuiondoshea vikwazo Sudan halitosuluhishwa hivi karibuni kwa sababu uamuzi upo katika mikono ya Bunge na sio utawala wa Trump kwa mujibu wa Gazeti la Elaph lililochapishwa mnamo Jumatano 04/09/2019. Kwa maana Marekani ilikuwa na msimamo mgumu katika kutumia vikwazo kama kadi ya kuishinikiza serikali ya Hamdouk, licha ya kwamba Amerika ilimuahidi Al-Burhan tokea mwanzo kwamba ingeondosha vikwazo. Al-Burhan alisema wakati huo, ("Kuna muendelezo wa mikakati kuhusiana na faili ya vikwazo tangu utawala wa zamani, tumetumana wajuzi wa kisheria kujadiliana suala hili na utawala wa Amerika…Amerika imeahidi kuiondosha Sudan kutoka katika orodha ya dola zinazodhamini ugaidi baada ya kukamilika mchakato wa amani na tunaamini kwamba huu ni wakati mzuri. Alisema: "Makubaliano yanaweza kutiwa saini wikendi hii baada ya kuandika mswada wa Muundo wa Serikali ya Mpito"… Middle East 7/7/2019). Ubalozi wa Amerika ndani ya Khartoum Steven Koutsis mnamo 7/7/2019 aliweka wazi kwamba (suala la kuiondosha Sudan kutoka katika orodha ya dola zinazodhamini ugaidi ni lakutarajiwa… Gulf Online on 7/7/2019).

c- Taasisi za Kifedha za Kimataifa (IMF na World Bak) zinaweza kutoa mikopo kwa Sudan kwa idhini ya Amerika. Hii ni kadi nyingine ya shinikizo iliyomo katika mikono ya Amerika na timu yake ya ndani. Pia, kwa sababu Sudan imebakia katika orodha ya Marekani ya ugaidi, hii inainyima kuweza kutumia nidhamu ya malipo ya kimataifa ya Amerika ambayo ni kikwazo kikubwa kwa biashara za kimataifa za Sudan ambapo ufanyaji biashara unategemea dolari.

Ama kuhusu Ulaya na hivyo basi Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko, kwa hiyo inatarajiwa itafuata michoro miwili: kwanza, kutegemea kwa Ulaya kupambana na "suala la vikwazo na kuchelewesha kwa Amerika kuiondoshea vikwazo," na kisha shinikizo la kiuchumi kama natija yake… Pili ni kuwahangaisha wanajeshi na vitengo vya usalama katika migao ya bajeti kifedha.

Kwanza, Ulaya "na hivyo basi Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko wanafahamu uzito wa athari ya vikwazo kwa uchumi wa Sudan, na pia wanazingatia kwamba Amerika itaendelea kuIshinikiza, hivyo basi itafanyakazi kuisadia serikali ya Sudan ndani ya Umoja wa Mataifa na kuipa msaada wa kifedha… Ujerumani imeandaa kuwasaidia; Waziri wa Kigeni Haikou Mas alisema ("nchi yake itazungumzia suala la kuiondosha Sudan kutoka katika orodha ya dola zinazodhamini ugaidi huko Baraza la Umoja wa Mataifa litakalofanyika mwezi huu"…Anadolu 8/9/2019). Waziri wa Kigeni wa Ufaransa (Le Drian) alizuru Khartoum mnamo 16/9/2019 na kukutana na Rais Abdullah Hamdouk na kusema: ("Nilimwambia Waziri wa Kigeni tutafanyakazi na washirika wetu wa Ulaya kuiondosha Sudan kutoka katika orodha ya Amerika ya dola zinazodhamini ugaidi" na kuongeza: "Ufaransa itaipa Sudan msaada wa ki-

**Endelea...UK 15**

wango cha Uro milioni 60. Uro milioni 15 zitapeanwa mara moja kwa wakati huu," ukurasa wa tovuti ya Sudanese Al-Rakouba 16/9/2019). Hii inaonyesha msaada kwa Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko na serikali ya Hamdouk.

La pili linajumuisha vitu viwili: kupunguza mgao wa bajeti kwa jeshi na kuleta mabadiliko katika huduma za usalama. Kauli ya Hamdouk inaashiria wazi hili:

Ama kuhusu bajeti, Hamdouk alitaka kuwepo na "kupunguzwa kukubwa katika matumizi ya jeshi… Akaongeza kwamba "matumizi ya jeshi yanachukua asilimia 80 ya bajeti ya dola" (Arabic Post 26/8/2019) akijadili kwamba kutiwa saini kwa makubaliano ya amani na harakati za kijeshi zilizosambaa nchini lazima "zirudi katika amani" kwa maana kuwa ili kupunguza matumizi ya kijeshi katika bajeti ya Sudan kwa jeshi na usalama.

Ama kuhusu mabadiliko katika huduma za usalama, muundo wa sasa wa huduma za usalama na jeshi ndani ya Sudan hususan hali ya Vikosi vya Msaada wa Haraka ambavyo viliundwa na utawala wa al-Bashir na vilitekeleza unyama mkubwa juu ya waandamanaji wa Sudan. Hivyo basi, kulikuwepo na uhalalishaji wa Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko kudai kubadilishwa kwa muundo wa vitengo hivyo ili kuhakikisha kuwa dola inavidhibiti na kwamba vifuate sheria, (Hamdouk alifichua kwamba Vikosi vya Msaada wa Haraka vitaunganishwa na huduma za usalama katika mchakato wa mageuzi ya muundo na kubuniwa kwa jeshi la kitaifa kwa ajili ya nchi. Aliongezea kwamba serikali yake iko makini kubadilisha muundo wa vitengo vya usalama ikijumuisha Msaada wa Haraka na majeshi ya harakati nyengine za kisilaha ili kuweza kujenga jeshi lenye nguvu la kitaifa. Al Jazeera Net 11/9/2019).

6- Inaonekana kwamba nafasi ya juhudi za Ulaya kutoa msaada kwa Majeshi ya Uhuru na Mabadiliko yamefaulu kuchache kuliko yale ya Amerika na wafuasi wake kutokana na nukta zifuatazo:

- Ama kuhusu msaada wa Ulaya hausuluhishi tatizo lolote. Lau Amerika haitoiondosha Sudan katika orodha ya dola zinazodhamini ugaidi itaendelea kutaabika, kama alivyosema Waziri Mkuu mwenyewe. Inategemea msaada wa kigeni ambao ni msaada ulio na riba ambao unaendelea kuikandamiza nchi na wawekezaji na hauwezi kuleta mapinduzi ya kiviwanda na hauwezi kuleta maendeleo katika rasilimali za uchumi wake. Ni ya uhalisia ule ule wa ufisadi ambao uko mbali na mfumo na Dini ya kweli ya Ummah ambao nidhamu hupichuza kutoka kwayo, na ambayp itaifufua nchi. Mtazamo wa kiuchumi ndio sababu kubwa uliopelekea mapinduzi dhidi ya utawala wa Al-Bashir kwa kuwa watu wengi wanaangamia katika umasikini, kunyimwa, ukosefu wa ajira na bei za juu.

- Ama kuhusu kupunguza bajeti ya jeshi, jeshi kwa miongo mingi limekuwa likichukua mgao mkubwa wa bajeti ya Sudan na inatarajiwa kupinga vikali upunguzaji huo kwa njia tofauti tofauti ili kuhalalisha kuwepo kwa matumizi makubwa… Ama kuhusu ufisadi wa kifedha pande zote mbili hazijanusurika kwa hivyo nani kati yao atatatua suala hilo?! Ufisadi wa kifedha unasuluhishwa tu na wanaume wanaomuogopa Mwenyezi Mungu na kuongozwa na Uislamu katika hukmu zake zote sio chini ya nidhamu iliyowekwa na mwanadamu.

- Ama kuhusu huduma za usalama, Amerika imejifunga na mtu mmoja naye ni Mohammad Hamdan Dagalo (Himaidti), kamanda wa Vikosi vya Msaada wa Haraka ambaye amezidisha kauli zake na ziara zake hususan kuelekea Misri na Saudi Arabia. Inaonekana kwamba ndiye chaguo la Amerika la siku zijazo kwa Sudan, Himaidti, naibu mwenyekiti wa Baraza la Ubwana, atakuwa kipingamizi kwa mabadiliko katika Vikosi vya Msaada wa Haraka ambavyo kwa mujibu wa baadhi ya vyanzo vinajumuisha takribani asilimia 25 ya bajeti ya jeshi. Hivyo basi juhudi za serikali ya Hamdouk kuunda upya huduma za usalama ndani ya Sudan moja kwa moja zitagongana na mwanamume anayeungwa mkono na Amerika ndani ya Sudan, Himaidti!

7- Hivyo basi, hali ya kisiasa na kiuchumi ndani ya Sudan haitarajiwi kumakinika wakati wa muhula wa mpito:

- Ama utulivu wa kisiasa haupatikani ndani ya nchi kwa sharti kuna mzozo wa kimataifa ambao unachochewa na zana za kindani. Hili liko wazi kwa mabalozi wa harakati za kimataifa ndani ya Sudan na kutoka kwa kauli zao, vitendo vyao na mikutano yao na maafisa wa kindani kama ilivyo onyeshwa hapo juu. Hivyo basi utulivu hautopatikana na inawezekana ukosefu wa amani kupelekea mapinduzi ya kijeshi ndani ya muhula wa mpito kwa msaada wa Amerika labda watu wa Sudan watambue uhalisia huu na wampe nusra Mwenyezi Mungu (swt) kwa kuondosha makafiri waliokoloniwa kutoka katika mizizi popote walipo na washirika wao… Na wasimamishe utawala wa Kiislamu, Khilafah Rashida (Khilafah iliyoongoka) kwa njia ya Utume. Watakuwa washindi na wataweza kuishi kwa usalama katika nyumba zao na kurudi kwa Mwenyezi Mungu kama walivyotarajiwa wawe:

**(خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ)** "Umma bora walio tolewa watu" [Al-i-Imran: 110].

- Ama kuhusu ukosefu wa utulivu wa kiuchumi ni

**Endelea...UK 16**

natija ya uingiliaji wa kikoloni ndani ya nchi, hauwezi kuvuna zabibu kutoka katika miba! Sudan Kusini imetenganishwa na utajiri wa mafuta umepotezwa kwa maagizo ya Amerika kwa mtawala aliyeusaliti Ummah katika hilo. Sudan, kama ilivyoelezewa kuwa ni kapu la chakula cha Afrika, watu wake wamekuwa masikini wa kupindukia kwa sababu ya kutegemea mikopo ya riba na ardhi zao zimekosa misaada kwa wakulima na kuwatafutia soko bidhaa zao kwa hivyo wakaachana nazo. Utajiri wa madini ukawachiwa uwekezaji wa kigeni na kuendelea hivyo… Na kisha la muhimu zaidi, Uislamu ukaondoshwa madarakani na nidhamu ya kiuchumi ndani ya Uislamu ikatelekezwa ambayo imewekwa na Mwenyezi Mungu (swt) na nidhamu fisadi ya wanadamu ikatelekezwa, itawezekanaje kupatikane utulivu wa kiuchumi? Bali kutakuwepo na maisha ya dhiki na Mwenyezi Mungu Al-Aziz Al-Hakim, ndiye Msema kweli anayesema:

**(فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَى * وَمَنْ أَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكاً)**

“Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika* Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki” [Ta-Ha: 123-124].

**24 Muharram Al-Haram 1441 H**
**23/9/2019 M**